

Jarida hili linaripoti na kuchunguza matokeo ya utafiti usiotumia takwimu bali ujuzi na mitazamo ya watu juu ya matumizi ya istilahi za saratani katika mji wa Bagamoyo, Tanzania. Kufuatia wito wa hivi karibuni wa kukusanya ushahidi pamoja na vitendo vya kimaadili katika sekta ya afya kimataifa, utafiti huu unawaangazia wanaisimu-jamii kama watu muhimu wa kuingia na kufuma elimu hii ya ufahamu ili kufahamu vyema utekelezaji wa shughuli za afya ya umma.

Tulitumia mahojiano aina ya ethnografia ili kufichua mifumo ya muktadha na mifuatano inayohusiana na matumizi ya istilahi za saratani kwa wakazi wa Kata ya Dunda mjini Bagamoyo kwa upana. Matokeo yetu yanaonyesha kuwa watu wa Bagamoyo hutumia istilahi mbalimbali kuelezea na kutengeneza tafsiri juu ya saratani ambayo haiendani vizuri na dhana za kimatibabu.

Utafiti huu sio tu unafungua uchunguzi zaidi juu ya jinsi watu wa kawaida wanavyozungumza na kulielewa janga la saratani linalojitokeza katika maeneo kama Tanzania, lakini pia ni dirisha la dhana nyingine ya kufuma mikakati katika nchi zilizowahi kutawaliwa ili kuboresha hali ya afya. Tunasema kuwa kurekebisha dhana za kimatibabu katika isimu-jamii na miundo ya maarifa ni kazi muhimu katika kujenga msingi wa maadili, vitendo vinavyotoa taarifa za uhakika katika sekta ya afya kimataifa.